Khutba ya Kwanza

الإستجابة لله ولرسوله

# KUMUITIKIA MWENYEZI MUNGU NA MTUME WAKE

**Imefasiriwa**

**Na**

**Profesa Ayman Alasar**

**kitivo cha lugha na ufasiri**

**Assalaam Alaikum Warahmatullah Wabarakatuh.**

Shukrani zote anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote. Msemaji ndani ya Kitabu chake:

**اسْتَجِيبُوا لِرَبِّكُمْ مِنْ قَبْلِ أَنْ يَأْتِيَ يَوْمٌ لَا مَرَدَّ لَهُ مِنَ اللَّهِ مَا لَكُمْ مِنْ مَلْجَإٍ يَوْمَئِذٍ وَمَا لَكُمْ مِنْ نَكِيرٍ**

{**Muitikieni Mola wenu Mlezi kabla haijafika siku isiyoepukika itokayo kwa Mwenyezi Mungu. Siku hiyo hamtakuwa pa kukimbilia wala hamtakuwa na cha kukingia**} pia Amesema:

**لِلَّذِينَ اسْتَجَابُوا لِرَبِّهِمُ الْحُسْنَى** {**Walio muitikia Mola wao Mlezi watapata wema**}. Ninashuhudia kuwa hakuna mola wa haki isipokuwa ni Mwenyezi Mungu peke yake hana mshirika, na ninashuhudia kuwa Mtume wetu Muhammadi ni mja wake na Mtume wake. Ewe Mwenyezi Mungu peleka rehma na amani kwake na kwa watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake na wale wote wenye kumfuata kwa wema mpaka siku ya malipo.

**Baada ya Utangulizi**:

Mwenye kuzingatia kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu atakuta wito wa wazi wa maisha bora yenye furaha, na uwokozi duniani na Akhera kwa kumuitikia Mwenyezi Mungu na Mtume wake S.A.W ambapo anasema Mola wa haki:

**يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اسْتَجِيبُوا لِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ.**

{**Enyi Mlioamini, muitikieni Mwenyezi Mungu na Mtum**} na anaendelea kusema:

أَوَمَنْ كَانَ مَيْتًا فَأَحْيَيْنَاهُ وَجَعَلْنَا لَهُ نُورًا يَمْشِي بِهِ فِي النَّاسِ كَمَنْ مَثَلُهُ فِي الظُّلُمَاتِ لَيْسَ بِخَارِجٍ مِنْهَا.

{**Je, aliye kuwa maiti kisha tukamhuisha na tukamjaalia nuru inakwenda naye mbele za watu, mfano wake ni kama aliyoko gizani akawa hata hawezi kutoka humo?**} na anasema tena:

مَنْ عَمِلَ صَالِحًا مِنْ ذَكَرٍ أَوْ أُنْثَى وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَلَنُحْيِيَنَّهُ حَيَاةً طَيِّبَةً وَلَنَجْزِيَنَّهُمْ أَجْرَهُمْ بِأَحْسَنِ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ.

{**Mwenye kutenda mema, mwanamume au mwanamke, naye akawa ni Muumini, tutamhuisha maisha mema; na tutawapa ujira wao kwa bora ya waliyo kuwa wakiyatenda**}.

Hakuna shaka kuwa kumuitikia Mwenyezi Mungu na Mtume wake S.A.W ni njia ya Waumini wa kweli waliowezeshwa kushukuru neema za Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutumia viungo ambavyo Mwenyezi Mungu amewapa ili kumsikia Mwenyezi Mungu wa kweli na kumuitikia, ambapo Anasema Mola Mtukufu:

إِنَّمَا يَسْتَجِيبُ الَّذِينَ يَسْمَعُونَ.

{**Hakika wanaoitikia ni wale wanao sikia**}.

Kama vile kuitikia ni jambo la Manabii walioteuliwa na Malaika waliokaribu, pindi Mwenyezi Mungu alipomuamrisha Mtume wake Nuh A.S kutengeneza jahazi jangwani ambapo hamma mto wala bahari aliitikia na kutekeleza amri ya Mola wake Mtukufu, ambapo Mola Mtukufu Anasema:

وَاصْنَعِ الْفُلْكَ بِأَعْيُنِنَا وَوَحْيِنَا وَلَا تُخَاطِبْنِي فِي الَّذِينَ ظَلَمُوا إِنَّهُمْ مُغْرَقُونَ * وَيَصْنَعُ الْفُلْكَ وَكُلَّمَا مَرَّ عَلَيْهِ مَلَأٌ مِنْ قَوْمِهِ سَخِرُوا مِنْهُ قَالَ إِنْ تَسْخَرُوا مِنَّا فَإِنَّا نَسْخَرُ مِنْكُمْ كَمَا تَسْخَرُونَ.

{**Na unda jahazi mbele ya macho yetu na kwa mujibu wa ufunuo wetu. Wala usinisemeze kuwatetea waliodhulumu. Kwani hao bila ya shaka watazamishwa * Na akawa anaunda jahazi, na kila wakipita wakuu wa kaumu yake**

**wakimkejeli. Yeye akasema: Ikiwa nyinyi mnatukejeli na sisi tunakukejelini kama mnavyo tukejeli**}.

Pindi Mwenyezi Mungu alipomuamrisha Mtume wake Ibrahimu A.S kuwalingania watu Ibada ya Hija ambapo Mola Mtukufu Anaasema:

**وَأَذِّنْ فِي النَّاسِ بِالْحَجِّ يَأْتُوكَ رِجَالًا وَعَلَى كُلِّ ضَامِرٍ يَأْتِينَ مِنْ كُلِّ فَجٍّ عَمِيقٍ.**

{**Na watangazie watu Ibada ya Hija; watakujia kwa miguu na juu ya kila ngamia aliye konda, wakija kutoka katika kila njia ya mbali**}.

Muitikio wake ulikuwa pale alipomuambia Mola wake Mtukufu: Ewe Mola sauti yangu ni vipi itafika? Mola Mtukufu Akasema: **أَذِّنْ وعَلَيَّ البَلاغُ** Tangaza ni jukumu langu kuwafikia. Vile vile pale Mwenyezi Mungu alipomuamrisha kumchinja mtoto wake ikiwa kuitikia kwake na kujisalimisha kwa Mola wake pamoja na mtoto wake Ismaili A.S ambapo Mola Mtukufu Anasema:

**فَبَشَّرْنَاهُ بِغُلَامٍ حَلِيمٍ * فَلَمَّا بَلَغَ مَعَهُ السَّعْيَ قَالَ يَا بُنَيَّ إِنِّي أَرَى فِي الْمَنَامِ أَنِّي أَذْبَحُكَ فَانْظُرْ مَاذَا تَرَى قَالَ يَا أَبَتِ افْعَلْ مَا تُؤْمَرُ سَتَجِدُنِي إِنْ شَاءَ اللَّهُ مِنَ الصَّابِرِينَ * فَلَمَّا أَسْلَمَا وَتَلَّهُ لِلْجَبِينِ * وَنَادَيْنَاهُ أَنْ يَا إِبْرَاهِيمُ * قَدْ صَدَّقْتَ الرُّؤْيَا إِنَّا كَذَلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ * إِنَّ هَذَا لَهُوَ الْبَلَاءُ الْمُبِينُ * وَفَدَيْنَاهُ بِذِبْحٍ عَظِيمٍ.**

{**Basi tukambashiria mwana aliye mpole * Basi alipo fika makamo ya kwenda na kurudi pamoja naye, alimwambia: Ewe mwanangu! Hakika mimi nimeona usingizini kuwa ninakuchinja. Basi angalia wewe, waonaje? Akasema: Ewe baba yangu! Tenda unavyoamrishwa, utanikuta mimi, Inshallah, katika wanaosubiri * Basi wote wawili walipo jisalimisha, na akamlaza juu ya kipaji * Tulimwita: Ewe Ibrahim * Umekwisha itimiliza ndoto. Hakika hivi ndivyo tunavyo walipa wanao tenda mema * Hakika haya ni majaribio yaliyo wazi * Basi tukamtolea fidia kwa kichinjo kitukufu**}.

Maswahaba wa Mtume wamekuwa mfano bora katika kumuitikia Mwenyezi Mungu na Mtume wake S.A.W kwani ndani ya siku ya vita vya Hamraa Al-Asad Maswahaba waliitikia amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na amri ya Mtume wake S.A.W pamoja na kupatwa na majeraha na maumivu makali kutokana na yaliyotokea siku ya vita vya Uhud, hivyo Qurani Tukufu ikawaelezea kwa sifa nzuri

pale iliposema: الَّذِينَ اسْتَجَابُوا لِلَّهِ وَالرَّسُولِ مِنْ بَعْدِ مَا أَصَابَهُمُ الْقَرْحُ لِلَّذِينَ أَحْسَنُوا مِنْهُمْ وَاتَّقَوْا أَجْرٌ عَظِيمٌ {**Walio muitikia Mwenyezi Mungu na Mtume baada ya kwisha patwa na majeraha - kwa walio fanya wema miongoni mwao na wakamcha-Mungu utakuwa ujira mkubwa**}.

Na katika tukio la kugeuzwa Qibla kutoka Baitul-Maqdisi na kuelekea kwenye Kaaba Takatifu ulikuwa ni muitikio wa haraka kwa Maswahaba *Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe kwao* ambapo waligeuka wakiwa ndani ya ibada ya swala na walikuwa wanaswali wakiwa wameelekea Baitul-Maqdis – pindi alipokuja mtu na kuwafahamisha kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu S.A.W ameteremshiwa amri ya kuelekea Kaaba katika swala, vile vile muitikio wao R.A pale sura ya Mtume S.A.W ilipobadilika na kuanza kuwa na huzuni kwa kuwaona watu masikini hawana viatu wala mavazi, aliwaita Maswahaba zake R.A kutoa sadaka akisema: "***Mtu kutoa sadaka katika pesa zake nguo pishi ya ngono yake pishi ya tende zake mpaka akasema: Hata kama atatoa tunda moja ya tende***" akaja mtu katika watu wa Answar na maziwa mikono yake ilikaribia kushindwa kubeba kisha watu wakawa wanamfuata akitoa sadaka mpaka mwisho sura ya Mtume S.A.W ikiwa kuwa na tabasamu na furaha.

Na ilikuwa katika uitikiaji wa haraka wa Maswahaba wa Mtume wetu S.A.W katika kuacha yaliyoharamu kama vile uharaka wao wa kuitikia utiifu na amri, ilipoteremka kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kuharamisha kabisa pombe:

**يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِنَّمَا الْخَمْرُ وَالْمَيْسِرُ وَالْأَنْصَابُ وَالْأَزْلَامُ رِجْسٌ مِنْ عَمَلِ الشَّيْطَانِ فَاجْتَنِبُوهُ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ.**

{**Enyi mlio amini! Bila ya shaka ulevi, kamari, kuabudu masanamu na kupiga ramli, ni uchafu katika kazi ya Shetani. Basi jiepusheni navyo ili mpate kufanikiwa**}. Maswahaba wa Mtume S.A.W wakasema tumeacha Ewe Mola wetu tumeacha Ewe Mola wetu.

*****

**Khutba ya Pili**

Shukrani anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, rehma na amani zimuendee Mtume wa mwisho naye ni Mtume wetu Muhammad S.A.W pamoja na watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake wote.

Mwenyezi Mungu Mtukufu amewakirimu msamaha uwokuvu na Pepo siku ya Kiyama watu wenye kumuitikia Mwenyezi Mungu na Mtume wake S.A.W ambapo Mwenyezi Mungu Anasema:

يَا قَوْمَنَا أَجِيبُوا دَاعِيَ اللَّهِ وَآمِنُوا بِهِ يَغْفِرْ لَكُمْ مِنْ ذُنُوبِكُمْ وَيُجِرْكُمْ مِنْ عَذَابٍ أَلِيمٍ.

{**Enyi watu wetu! Muitikieni Mwenye kuitia kwa Mwenyezi Mungu, na muaminini, Mwenyezi Mungu atakusameheni, na atakukingeni na adhabu chungu**}, kwa sababu malipo ni sawa na matendo kwani Mwenyezi Mungu anaitikia maombi ya wanaoitikia amri zake, ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu Anasema:

وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِي عَنِّي فَإِنِّي قَرِيبٌ أُجِيبُ دَعْوَةَ الدَّاعِ إِذَا دَعَانِ فَلْيَسْتَجِيبُواْ لِي وَلْيُؤْمِنُواْ بِي لَعَلَّهُمْ يَرْشُدُونَ.

{**Na waja wangu watakapo kuuliza habari zangu, waambie kuwa Mimi nipo karibu. Na itikia maombi ya muombaji anapo niomba. Basi na waniitikie Mimi, na waniamini Mimi ili wapate kuongoka**}.

Na anasema tena: فَاسْتَجَابَ لَهُمْ رَبُّهُمْ أَنِّي لاَ أُضِيعُ عَمَلَ عَامِلٍ مِّنكُم مِّن ذَكَرٍ أَوْ أُنثَى {**Mola Mlezi wao, akayakubali maombi yao akajibu: Hakika sipotezi kazi ya mfanyakazi miongoni mwenu, akiwa mwanamme au mwanamke**}.

Na anaendelea kusema:

وَقَالَ رَبُّكُمُ ادْعُونِي أَسْتَجِبْ لَكُمْ إِنَّ الَّذِينَ يَسْتَكْبِرُونَ عَنْ عِبَادَتِي سَيَدْخُلُونَ جَهَنَّمَ دَاخِرِينَ.

{**Na Mola wenu Mlezi anasema: Niombeni nitakuitikieni. Kwa hakika wale ambao wanafanya kibri kuniabudu Mimi wataingia Jahannamu wadhalilike**}.

Ni kwa namna gani tunahitaji kumuitikia Mwenyezi Mungu Mtukufu na Mtume wake S.A.W kwani hiyo ndio njia ya Waumini wa kweli ambapo Mola Anasema:

إِنَّمَا كَانَ قَوْلَ الْمُؤْمِنِينَ إِذَا دُعُوا إِلَى اللَّهِ وَرَسُولِهِ لِيَحْكُمَ بَيْنَهُمْ أَنْ يَقُولُوا سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ.

{**Haiwi kauli ya Waumini wanapoitwa kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake ili ahukumu kati yao ila ni kusema: Tumesikia na tumetii! Na hao ndio wenye kufanikiwa**}.

Ewe Mwenyezi Mungu tunakuomba uhifadhi Misri pamoja nchi zengine duniani.

**Wassalaam Alaikum Warahmatullah Wabarakatuh**